

# HALMASHAURI YA WILAYA YA NSIMBO

Barua pepe:info@nsimbodc.go.tz  
Tovuti:www.nsimbodc.go.tz



S.L.P 688

MPANDA

Press No: NDC/ICPRU/Press no.13

June 11, 2018

## TAARIFA KWA UMMA/VYOMBO VYA HABARI

### TAHADHARI YA UGONJWA WA EBOLA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo **Bw.Mwailwa Smith Pangani** anawatangazia wananchi wote wa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo na Katavi kwa ujumla kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa hatari wa Ebola.

Licha ya kutokuwa na taarifa rasmi ya Ugonjwa huo kuingia Nchini **Mkurugenzi Mwailwa** anawataka wananchi wote wa Nsimbo na Mkoa wa Katavi kwa ujumla kuchukua tahadhari ikiwa ni pamoja na kuwa makini na wageni hususani Wafanyabiashara wanaoingia Nchini kutoka Nchi jirani ya Kongo iliko Ebola kwa sasa kwa kuwa muingiliano huo huenda ukawa sababu kubwa ya kuingia rasmi na kuenea kwa Ugonjwa huo hatari hapa Nchini.

Ugonjwa wa Ebola ni Ugonjwa hatari unaosababishwa na virusi aina ya Ebola Virus unaoambukizwa kwa sehemu kubwa kwa kugusana na majimaji ya mtu mwenye maambukizi ya Ebola ambapo mpaka sasa hakuna taarifa yoyote ya kuwepo kwa Tiba wala Kinga ya Ugonjwa huo.

Hivyo wananchi wanashauriwa kuchukua tahadhari kwa kuepuka kabisa kugusana majimaji ya mwili na mtu mwenye maambukizi ya Ebola kwani huchangia kwa kiasi kikubwa kuenea kwa maambukizi ya Ugonjwa huo.

Aidha Mwananchi anasisitizwa kutoa taarifa kwa Uongozi ama kumwona Daktari haraka katika kituo chochote cha Afya ama Zahanati endapo atakuwa na dalili ama kuona mtu mwenye dalili zifuatazo;

- Kuumwa na kichwa kunakoambatana na homa kali ya ghafla
- Kulegea mwili
- Vidonda vya koo
- Kutapika kunakoambatana na kuhara
- Vipele vya ngozi
- Kutoka damu puani,mdomoni machoni na njia ya haja kubwa

Mpaka sasa ugonjwa huo umeripotiwa kuenea na kusababisha vifo vya watu kadhaa Nchini Kongo ambapo jitihada za Serikali nchini humo kwa kushirikiana na Mashirika na Asasi za Kiraia zinaendelea ili kudhibiti na kukomesha kabisa maambukizi ya ugonjwa huo.

**Imetolewa na :**



*John A. Mganga*

**Afisa Habari Mawasiliano na Uhusiano (W)  
Kitengo cha Habari Mawasiliano TEHAMA na Uhusiano,  
Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo.**